**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**MKOA WA NJOMBE**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

**SHULE YA SEKONDARI WANIKE,**
**100 KITONGOJI CHA SADANI**
**59301 MDANDU-WANGING'OMBE**
**S. L. P 358**
**NJOMBE**
**13/05/2026**

Simu namba:

**Mkuu wa Shule: 0762055083 / 0768256129**

**KUMB.NA.WSS/KDTV/ADMN/2026/2027**

**JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………………….**

**S.L.P …………………………………………………………………………………………..**

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WANIKE HALMASHAURI YA WANGING'OMBE, MKOA WA NJOMBE MWAKA 2026/2027.**

Ninafuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2026/2027** Kabla ya kuripoti hakikisha unafanyiwa uchunguzi wa afya yako katika hospitali ya wilaya au mkoa na kujaziwa fomu maalumu na mganga mkuu. Fomu imeambatanishwa. Pia unatakiwa kujaza fomu ya kukubali kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na kuandika mawasiliano sahihi ya mzazi au mlezi katika sehemu husika.
Hutapokelewa bila kutimiza maagizo yaliyoorodheshwa kwenye fomu hizi.

## MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya sekondari Wanike ipo mkoa wa Njombe wilaya ya Wanging'ombe, kata ya Mdandu. Shule ipo kilometa 30 kutoka Njombe mjini na kilometa 40 kutoka Makambako. Ukifika Makambako panda magari yanayoelekea Igwachanya kupitia Mdandu nauli hadi kibao cha shule ni **Tsh.6000/= AU** Ukifika Njombe panda magari yanayoelekea Igwachanya kupitia Mdandu, nauli kutoka Njombe

mjini ni **Tsh.5000/=.** shuka kwenye kibao cha Wanike sekondari, panda pikipiki hadi shuleni kwa **Tsh. 2000/=** ambapo pana umbali wa kilometa tatu(3) .Magari hayo yote yanaondoka saa saba mchana.

**SARE ZA SHULE.**

**WASICHANA**

**a) Sare ya darasani.**

i. Sketi mbili rangi ya darkblue mshono rinda boksi (marinda mawili) kitambaa namba moja cha suti ushone mwenyewe na iwe **ndefu(sm 20 kutoka kwenye unyayo)**.

ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu (tomato)

iii. Sweta dark blue.

iv. Viatu pea mbili vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi.

v. Soksi jozi mbili nyeupe zisizo na maua yoyote.

vi. Neck tie ya rangi ya darkblue.

vii. Tisheti ya rangi ya blue yenye kola nyeupe na mfuko upande wa kushoto isiyo na maandishi yoyote.

**b) Sare za kazi.**

i. Sketi ya rangi nyeusi mshono wa rinda boksi kitambaa namba moja cha suti.

ii. Tisheti rangi ya kijivu isiyo na maneno yoyote na yenye kola.

iii. Track suit rangi ya blue bahari.

**c) Sare za michezo.**

i. Jezi rangi nyekundu isiyo na maandishi kwa tahasusi zote.

ii. Bukuta rangi nyekundu.

iii. Raba rangi nyeupe kwa wote.

iv. Soksi ndefu zinazofanana na jezi yako ya juu zifike magotini.

**d) Kwa watakao vaa hijabu.**

i. Darasani juba rangi nyeupe inayoishia kifuani. ii. Kazini juba rangi nyeusi inayoishia kifuani.

**WAVULANA**

**i. SARE ZA DARASANI .**

a. Suruali mbili rangi ya dark blue yenye turn up yenye upana unaostahili (isiyo bana) ishonwe hukohuko.

b. Mashati mawili meupe mikono mirefu (tomato).
c. Sweta rangi ya dark blue moja au zaidi.
d. Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vyenye kamba.
e. Soksi jozi mbili nyeusi zisizo na maua.
f. Tai ya kufunga rangi ya dark blue.
g. T-shirt rangi ya bluu yenye kola nyeupe na mfuko upande wa kushoto isiyo na maandishi yoyote.

ii. **SARE ZA KAZI.**

a. Suruali rangi nyeusi yenye turn up yenye upana unaostahili.(isiyo bana) ishonwe hukohuko.
b. Tisheti rangi ya kijivu isiyo na maneno yoyote na yenye kola.
c. Track suit rangi ya blue bahari.

iii. **SARE ZA MICHEZO.**

a. Jezi rangi nyekundu isiyo na maandishi.
b. Bukta rangi nyekundu.
c. Viatu vya michezo vizuri kulingana na mchezo unaopendelea kucheza na kuuweza.

**N.B: HURUHUSIWI KUJA NA NGUO NJE YA ZILE ZILIZOAGIZWA, UKIKIUKA AGIZO HILI UTAPEWA ADHABU KALI NA TUTACHOMA NGUO ZOTE AMBAZO HAZITAKIWI MBELE YAKO.**

**MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI.**

Hakikisha unapokuja unakuja na vitu vifuatavyo;

i. Godoro **$2^{1/2}$ x 6.**

ii. Tranka moja kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake iii. Mashuka mawili rangi ya blue bahari. iii. Blanketi moja.

iv. Kanga mbili au vitenge pamoja na taulo kwa wasichana na taulo kwa wavulana.

v. Ndoo mbili rangi ya damu ya mzee

vi. Vyombo vya chakula kama vile sahani bakuri kijiko na kikombe.

vii. Ream mbili(2) za karatasi (A4) aina ya **paper line**

viii. viii. Madaftari makubwa (counter books) 3quire ya kutosha kwa masomo yake yasiyo pungua kumi na tatu (13) au Zaidi na begi la kubebea madaftari

ix. File moja kwa ajili ya kutunzia taarifa zako ofisini. x. Nguo za ndani za kutosha .

xi. Mathematical set (mkebe), peni za kutosha penseli na rula.

xii. Scientific calculator kwa wale watakaosoma masomo ya **physics, mathematics na Geography.**

xiii. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika anayosoma mwanafunzi.

xiv. Kila mwanafunzi aje na nakala ya matokeo yake ya kidato cha nne.(Result slip) asipokuja nayo hatapokelewa.

xv. Kila mwanafunzi aje na nakala ya cheti chake cha kuzaliwa.

xvi. Kwa wanafunzi wa **PGM** waje na sululu moja lenye mpini , pamoja na squizer moja kwa ajili ya kukaushia sakafu, wanafunzi wa **HGK na HGFa** waje na shoka moja lenye mpini, panga moja pamoja na fagio (soft bloom) moja na wanafunzi wa **HKL na HGLi** waje na spade, panga moja pamoja na hard bloom moja ya kusugulia sakafu.

**MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE.**

a. Uendeshaji wa shule Tsh. **65,000/=**
b. Tahadhali Tsh. **5,000/=**
c. Kitambulisho cha mwanafunzi Tsh.**5000/=**
d. Nembo **Tsh. 5,000/=**

## Jumla Tsh. 80,000/=

**MICHANGO YOTE HIYO YA FEDHA ILIPWE KUPITIA BENKI YA NMB NA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NA RISTI ZA MALIPO YA BENKI**
**(ORIGINAL PAY IN SLIPS) Pia hakikisha yanaandikwa majina matatu ya mwanafunzi anayelipa hiyo michango.**

Jina la benki: **NMB.**
Jina la akaunti: **WANIKE SECONDARY SCHOOL.** Akaunti namba. **60601000012**

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi wa aina yoyote ile.

ii. Kugoma au kuhamasisha mgomo.

iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.

iv. Kupigana

v. Kusuka nywele.

vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya. vii. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja na kuolewa. viii. Kupata ujauzito au kutoa mimba.

ix. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.

x. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi pamoja na vifaa vingine vya umeme katika mazingira ya shule.**

xi. Kudharau bendera ya taifa.

xii. Kufanya jaribio lolote la kuua au kujiua kama kunywa sumu na kadhalika.

xiii. Uhalibifu wa mali ya umma kwa maksudi

**MIPAKA YA MWANAFUNZI AKIWA SHULENI.**

i. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule.

ii. Ni kosa kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum

a. Chumba cha walimu (staff room)
b. Ofisi za shule.
c. Maabara.
d. Jikoni.
e. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

iii. Ni kosa kubaki bwenini muda wa darasani bila kibali maalumu.

**MAWASILIANO KIUJUMLA.**

**a. Ofisi ya mkuu wa shule.**
**0762055083**
**0768256129**

**b. Ofisi ya taaluma.**
**0755 315703**
**0768717373**


**c. Ofisi ya uhasibu. 0766 36 60 58**

**d. Ofisi ya malezi**
**0766139056**

**NB: PIGA AU TUMA UJUMBE MFUPI ( kueleza shida yako na ujitambulishe)**

# KARIBUNI SANA WANIKE SEKONDARI

***"EDUCATION IS THE MILL FOR SUCCESS"***




**SHULE YA SEKONDARI WANIKE. FOMU YA KUKUBALI.**

1. **SEHEMU YA MWANAFUNZI. A. KUJIUNGA NA SHULE HII.**

Mimi …………………………………………………………………………………… Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha tano mwaka 2026 katika shule ya sekondari wanike na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na elimu ya kujitegemea.

MAHALI UNAPOISHI…………………………………………………………………

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………

TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………………………

**B. KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi

……………………………………………………………………………………………

Mwanafunzi wa kidato cha tano, tahasusi ya ……………. Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi na familia yangu kwa ujmla, kuwa sitashiriki au kuchochea fujo , mgomo na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shuleni na nyumbani nitakuwa raia mwema na mzalendo kwa nchi yangu.

**Saini…………………………………………….**

**Tarehe…………………………………………..**

2. **SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.**

Mimi ………………………………………ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari wanike mwaka 2026 na ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Aidha ninahidi nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na taifa. Na nitafuatilia maendeleo yake

kitaaluma,tabia, mwenendo na nidhamu ya mtoto wangu nikishirikiana na walimu.

Anuani yangu ya kudumu ni ……………………………………………………
……………………………………………………………
……………………………………………………………
Namba ya simu……………………………………………………………………
Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi , ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini …………………………………………tarehe ………………………………

**NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)**

**MEDICAL EXAMINATION FORM.**

**WANIKE SECONDARY SCHOOL,**
**P.O BOX 358,**
**NJOMBE.**
**……………………**

**TO,**
**THE MEDICAL OFFICER,**
……………………………
…………………………… ……………………………

Please examine……………………………………………………………………
As to her/his fitness for pursuing further education at this school.

a. Haemoglobin…………………………………………………………………
b. P.V. bleeding…………………………………………………………………
c. (i) Sight………………………………………………………………………
   (ii Hearing……………………………………………………………………
d. Blood pressure………………………………………………………………
e. Urine for sugar and pregnancy test…………………………………………
f. Stool for routine examination………………………………………………
g. Asthma…………………………………………………………………………
h. Skin diseases…………………………………………………………………
i. Leprosy…………………………………………………………………………
j. Epilepsy…………………………………………………………………………
k. Pulmonary tuberculosis………………………………………………………
l. Deformity………………………………………………………………………

m. Mental problem…………………………………………………………………………

n. Comments………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE.**

**(To be completed by the medical Officer)** I have examined the above named and consider that she /he is mentally and physically fit for studies.

**Signature………………………………………………Date…………………………**

**Desination…………………………………………Stamp……………**

**NB:( Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)**